JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO- RUKWA

SHULE YA SEKONDARI MATAI,

S.L.P 75,

MATAI – KALAMBO.

TAREHE ...../2018

NAMBA ZA SIMU
MKUU WA SHULE – **0763857102/076443094(WATSAP)**
MAKAMU MKUU WA SHULE - **0765890282**
MHASIBU-**0757493346**
MWL. TAALUMA **- 0758282097**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI .....
.....
S.L.P .....
.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATAI HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO, MKOA WA RUKWA, MWAKA 2018.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2018** tahasusi ya .....Shule ya Sekondari **MATAI** ipo umbali wa kilometa **52** Kusini-Magharibi mwa mji wa **SUMBAWANGA** na kilometa **2** kutoka katikati ya mji wa **Mata**i. Usafiri wa basi kutoka mjini **SUMBAWANGA** unapatikana katika kituo cha cha mabasi **SOKOMATOLA STEND YA MKOA**. Nauli ni shilingi 2,500/=
   Muhula wa masomo unaanza tarehe **2/JULAI/2018** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe **2/JULAI/2018** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **16/JULAI/2018**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia;**
   2.1 : Sare ya shule
   (a) Sare ya shule hii ni (suruari rangi ya khaki moja na blue bahari moja zenye malinda mawili. Tunashauri ashonee shuleni kwa gharama ya tsh.38,000/ kwa Suruali zote mbili ili kuepuka utofauti wa mishono na rangi kwa KUWA VIJANA WENGI WANAPENDELEA MTINDO WA MODEL.Tumeambatisha kipande cha kitambaa).
   (b). Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu.
   (c). Sare ya michezo kwa shule hii ni tracksuit moja blue bahari, bukta moja, Raba rangi yoyote.
   (d). Viatu rangi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
   (e)Soksi jozi mbili nyeupe za shule

(f). Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi

(g). Sweta rangi ya blue.

(h). Nguo za kushindia ni T.shirt moja ya kola rangi damu ya mzee yenye nembo ya shule, zitanunuliwa kwa pamoja shuleni kwa gharama ya sh.13,000/= na t-shirt ya duaraTsh. 9,000/= na tracksuit nyeusi (atoke nayo).

(g). Tai mbili rangi kama ya sare za shule.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya maelekezo hapo juu. Na siku ya kupokelewa avae Tracksuit nyeusi.

2.**2 Ada na Michango ya Shule**

(a). Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipia kiasi cha shilingi 35,000.00 au kulipa Ada yote kwa maramoja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **6211100050**, MATAI SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION katika Benki ya NMB Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

(b**). Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni;**

(i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.

(ii)Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

(iii)Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

(iv)Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

(v)Shilingi 2,000/- nembo ya shule

(vi)Shilingi 10,000/- kwa ajili ya huduma ya kwanza (Tshs. 5,000/= na Bima ya Afya Tshs. 5,000/= (Wanafunzi washauriwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya CHF kikaya)

(vii)Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima Mock

(viii). Fedha ya tahadhari 5,000/= (Haitarejeshwa)

(ix). Tsh. 50,000/= Ada ya mtihani wa Taifa (Atalipa akiwa kidato cha sita).

Michango katika kipengele (b) iwekwe kwenye

Akaunti namba 6211100048 MATAI SECONDARY SCHOOL SELF RELIENCE)- NMB.

(c). Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;

(i). Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)

(ii). Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha iambatishwe)

(iii). Scientific calculator- kwa mwanafunzi wa uchumi (HGE)

(iv). Godoro futi 2 1/2 .

(v). Mashuka pair 2 blue bahari, blanketi 1, foronya 1, chandarua 1.

(vi). Kiti na meza ya chuma – kwa gharama ya tsh. Elfu Hamsini .

(vii). Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

(viii). Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko

(ix). Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 1 (soft bloom/mopa).

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

(i). Wizi.
(ii). Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(ii). Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv). Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v). Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
(vi). Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii). Kufuga ndevu.
(viii). Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya .
(ix). Uvutaji wa sigara.
(x). Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
(xi). Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xii). Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.
(xiii). Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiv). Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xv). Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi). Kudharau Bendera ya Taifa.
(xvii). Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii). Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

(a). Fomu ya Uchaguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya wazazi kukiri kukubaliana na sheria; kanuni kulipa Ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.
(d). Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi Shuleni pamoja na namba zao za simu.

5**. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya mkuu wa shule.....

Jina la mkuu wa Shule.....MR..KASUNGA J.J.S.....

Mhuri wa Mkuu wa Shule.....

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO
SHULE YA SEKONDARI MATAI

MKATABA.

Unatakiwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu.

SEHEMU A: MWANAFUNZI

Mimi ..... Nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote za shule. Nakubali/ sikubali nafasi hii na kuwa nitatumia uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii sheria, maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

SAHIHI.....
TAREHE: .....

SEHEMU B: MZAZI /MLEZI

Mimi .....Mzazi/mlezi wa .....Nimepokea taarifa ya mwanangu ya kujiunga na Shule ya Sekondari MATAI. Kwa kutambua umuhimu wa Elimu na wajibu wangu, naahidi kuwa muda wote mwanangu atakapokuwa Shuleni nitashirikiana na uongozi wa Shule kumlea mtoto kwa kufuata sheria, maagizo na kanuni zote za Shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya Shule, nitatekeleza yote yatakayotolewa na Shule na nitatoa Ada na michango mingine yote ya Shule iliyopitishwa kwa wakati.

SAHIHI:.....
TAREHE:.....

MATAI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 75,
KALAMBO - RUKWA.

DATE:.....
MEDICAL OFFICER:
.....
.....
.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above named as to His/ Her fitness as indicated below. Arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.
This certificate must be signed by a qualified medical officer of recognized Hospital
.....

MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with regard to:-

Skin:.....Abdomen .....
Eyes: .....Urine: .....
Teeth: ..... Hemoglobin: .....
Spleen: ..... Chest: .....

Any Disabilities:.....

I consider that:-
He is in good health free from infections, and fit to come to school

He is fit come to school after having:.....
Treatment for: .....

Name & Signature .....Date.....

MEDICAL OFFICER

SHULE YA SEKONDARI MATAI – KALAMBO

FOMU YA KUANDIKISHA HABARI ZA MZAZI.

Jina Kamili: .....

Tarehe ya Kuzaliwa: .....

Mahali pa kazi: .....

Dini: .....

Uraia: .....

Wilaya ya Nyumbani: .....

Simu ya Baba: .....

Simu ya Mama: .....

Simu ya Mtendaji wa Mtaa Au Kijiji: .....

Maelezo mafupi kuhusu Afya ya Mwanafunzi: .....

.....

.....

Nathibitisha kuwa Taarifa nilizotoa Hapo Juu Ni Kamili Na Kweli.